

Bibilia ya watoto
Inaleta

Yesu awachagua
wasaidizi kumi na
wawili



Kimeandikwa na: Edward Hughes

Kimeorodheshwa na: Byron Unger; Lazarus

Imerekebishwa na: E. Frischbutter; Sarah S.

Kimetafsiriwa na: Grace Chepkoech

Kimedhibitishwa na: Bible for Children
www.M1914.org

©2008 Bible for Children, Inc.

License: Kuna ruhusa ya kuchapa hadithi hii, lakini bila ya kuuza.



Yesu alitenda mambo ya ajabu. Aliponya magonjwa, aliwapa watu wenye shida amani moyoni na akilini mwao na alifunza neno la Mungu.



Halaiki ya watu ilimjia Yesu kwa usaidizi na uponyaji. Akaamua kuchagua watu kumi na wawili kutokana na wale waliokuwa wakimfuata, ili wamsaidie katika kazi ya Mungu.





Kama una amuzi la kufanya, je wewe umwomba Mungu? Yesu alifanya hivyo! Katika mlima mnyamavu alizungumza na Baba yake wa mbinguni. Yesu aliomba hadi jua ilipotua.






Yesu aliomba
usiku mzima
pia.




Asubuhi, Yesu akawaita wote waliokuwa wakimfuata - marafiki wote waliokuwa wakimhudumia na kumtii. Kutokana nao akawachagua kumi na wawili wasaidizi wa kipekee au mitume.



Wawili wa kwanza kuchaguliwa walikuwa mandugu,
Simioni Petro na Andrea. Waliwacha biashara yao
ya kufua samaki Yesu alipowaita iliwamfuata.



Yakobo na Yohana, wana wa
Zebedayo, pia walicha
biashara yao ya kufua
samaki.




Yesu pia aliwachagua Filipi, Batholomeo, Mathayo, Thomasi, Simioni wa Ziloti, Yakobo mwana wa Alfayo, Yuda ndugu ya Yakobo na Yuda Iskariote ambaye mwishowe alimsaliti Yesu.




Yesu alifunza kuwa kutii aliyoyasema ilikuwa kama
kujenga nyumba juu ya mwamba. Mvua ikinyesha na
mafuriko yakija nyumba
ile haitaanguka.



Lakini wasiotii neno lake ni kama kujenga nyumba juu ya mchanga. Mvua ikinyesha na mafuriko yakija nyumba ile itaanguka.



Amri zingine za Yesu hazikuwa rahisi. "Mtu akikupiga ushavuni wa kulia, mpe pia wa kushoto aupige," Alifunza. "Mpende adui wako." Watu wanaitaji usidizi wa Mungu kuishi kama Yesu.



Yesu aliwaambia watu waombe
kwa siri - wasijionyeshe
katika maombi mbele ya watu
kama wafarisayo wengine.



Yesu alisema Mungu
angewalisha na kuwavisha
watu waliomwamini. Jinsi
Mungu aliwapa ndege chakula na
kupea maua rangi za kupendeza,
angewapa waliomwamini
walichohitaji.




Yesu aliwafunza
wasaidizi wake
aliowachagua vitu vingi
siku hiyo. Alipomaliza,
mtu mwenye ukoma
akaja na kumwomba
Yesu amponye.



Yesu akamjibu, "Nitakuponya. Kuwa mzima sasa."
Watu walipokuwa wakitazama mtu yule mwenye
ukoma akawa safi. Alikuwa amepona!

Mwana wa Mungu peke
ndiye angeweza kutenda
yale. Wasaidizi wake
walijua kuwa walikuwa na
mwalimu wa ajabu.



Yesu awachagua wasaidizi kumi na wawili
Hadithi kutoka kwa Neno la Mungu, Bibilia,
inapatikana katika

Mathayo 4-7, Marko 1, Luka 6

"Kufafanusha maneno yako kwatia nuru."
Zaburi 119:130



Mwisho



Hii hadithi ya bibilia inatueleza kumhusu Mungu wetu wa ajabu aliyetuumba na anayetaka tumjue.

Mungu anajua tumetenda mambo mabaya, anayoyaita dhambi. Adhabu ya dhambi ni mauti, lakini Mungu anakupenda sana hata akamtuma mwana wake wa pekee, Yesu, Ili afe msalabani na aadhibiwe kwa dhambi yako. Alafu Yesu akafufuka na kuenda nyumbani mbinguni! Ukimwamini Yesu na kumwomba msamaha kwa dhambi yako, Atakusamehe! Yesu atkuja na kuishi ndani yako, na utaishi naye milele.

Kama unaamini huu ni ukweli, Sema haya kwa Mungu: Mpendwa Yesu, ninaamini kuwa wewe ni Mungu, na ulifanyika mtu ili ufe kwa ajili ya dhambi zangu, ili niwe na maisha mapya, na siku moja nitaenda kuwa nawe millele. Nisaidie nikutii na niishi kwa ajili yako kama mtoto wako. Amina.

Soma bibilia na uzungumze na Mungu kila siku! Yohana 3:16

